



# **Cambridge O Level**

---

**SWAHILI**

**3162/01**

Paper 1

**May/June 2020**

**3 hours**



You must answer on the enclosed answer booklet.

You will need: Answer booklet (enclosed)

---

## **INSTRUCTIONS**

- Answer **all** questions.
- Follow the instructions on the front cover of the answer booklet. If you need additional answer paper, ask the invigilator for a continuation booklet.

## **INFORMATION**

- The total mark for this paper is 100.
- The number of marks for each question or part question is shown in brackets [ ].

---

This document has **8** pages. Blank pages are indicated.

1 Translate the following passage into English:

Binti yangu Aziza ni shabiki mkubwa wa muziki wa rumba. Yeye anapenda hasa nyimbo za Remmy Ongala. Ongala alizaliwa Kongo lakini alihamia Tanzania miaka ya 1970. Huko aliunda bendi ya muziki iliyoitwa 'Super Matimila'. Ongala hakuimba tu, bali alipiga gitaa pia.

Alipenda kuimba nyimbo zilizohusu mada mbalimbali. Aliimba kuhusu umaskini, ubaguzi wa aina zote, maradhi na pia maisha ya kawaida ya kifamilia.

Watu waliipenda sana sauti yake na pia ujumbe wa nyimbo zake. Ingawa Remmy Ongala alivuma zaidi kwenye vipindi vya miaka ya 1980 na 1990, hadi sasa ana mashabiki wengi. Aziza aliniambia kwamba kila mwaka mnamo mwezi wa nane watu kutoka nchi tofauti huja Tanzania ili kusherehekea Tamasha la Muziki wa Ongala. Kwa hivyo, urithi wake unaendelea kuunganisha vizazi vyote kwa pamoja chini ya mbingu za Afrika ya Mashariki.

Tamasha hili limemfanya Aziza afikirie kuunda bendi yake mwenyewe ya rumba mjini kwake. Atawaingiza humo wanamuziki wanaotoka Uganda, Kenya na Tanzania.

[20]

**2** Translate the following passage into **Swahili**:

Every Saturday, my friends and I play football on the school field. Sometimes our families come to cheer us on. After each game, we all enjoy a cold drink, such as water or orange juice. These usually come in plastic bottles.

A few months ago, our headmaster announced that he was planning to ban the use of plastic at school as it causes a serious litter problem. We all agreed that it is important to protect the environment, but we didn't want to give up our cold drinks! So, my friends and I got together to think about some solutions. It wasn't easy and took a long time. A lot of research was needed.

Eventually, we found out about a Tanzanian student who had won an award for scientific innovation. He had developed a special machine that mixes plastic and sand to make bricks and tiles. We told our teachers about this invention. They were pleased and bought one of these machines for the school.

Now we have a special bin for plastic. When the bin is full, we transfer all the plastic into the machine and add sand. We sell the bricks and tiles that we make and use the profit to improve the school. This new system has made a big difference by significantly reducing the amount of litter at school.

We have now won an award for the cleanest school in the region. This has made us all very proud, as you can imagine!

[30]

**3** Read the text and answer the questions that follow in **Swahili**.

Wiki iliyopita shule yetu ilitembelewa na Bwana Musa. Yeye ni Mkenya na anafanya utafiti katika chuo kikuu huko Nairobi. Mada ya utafiti wake ni ‘matumizi ya mitandao ya kijamii kwa vijana’.

Alipofika tu, alianza kwa kutuuliza maswali yaliyokuwa na lengo la kuchunguza mienendo na matumizi yetu ya mitandao ya kijamii. Alitaka kujua wanafunzi wangapi huangalia simu zao za mkononi pale wanapoamka tu. Ikabainika kwamba asilimia kubwa kati yetu hufanya hivyo. Wengi wetu hufuatilia picha zinazobandikwa na husoma maoni ya watu tofauti kuhusu picha hizo. Bwana Musa akaongeza kusema kwamba ana uhakika wengi wetu huendelea kuangalia simu zetu za mkononi kila baada ya dakika chache. Hapo tena wanafunzi wengi walicheka huku wakikubaliana na maneno yake. Tena zaidi ya hapo, rafiki yangu Hadija aliongeza ‘ninapoamka tu hukuta nimeshatumiwa ujumbe kama kumi hivi kunitaka nitoe maoni kuhusu picha zilizobandikwa usiku uliopita!’ Hapo tulicheka tena tukikubaliana naye.

Bwana Musa alituuliza maswali mengi. Swali ambalo lilinifanya nitafakari kuhusu mambo yanayonivutia linahusu chakula. Aliuliza, ‘wanafunzi wangapi hupiga picha za vyakula kabla ya kuvila?’ Ilibidi ninyooshe kidole na kusema mimi hufanya hivyo. Nilimfahamisha kwamba, pale ninapotembelea mikahawa na kula vyakula vilivyopambwa vizuri, mimi hupendelea kuvipiga picha. Pia hufanya hivyo ninapoviona vyakula ambavyo hupikwa kwa nadra. Siku hizi hata mama yangu haturuhusu kula kabla ya yeye mwenyewe kupiga picha huku akitania ‘hakuna ruhusa ya kula kabla ya kuvipiga picha vyakula’.

Bwana Musa alitufahamisha kwamba, maisha tulioyazoea sasa ni tofauti kabisa na yale ya watu waliozaliwa miaka kumi au kumi na tano tu iliyopita. Vijana wa sasa hawathamini mazungumzo ya ana kwa ana na hawaandikiani barua kama zamani. Vijana wa sasa wanategemea mitandao ya kijamii ili kuwasiliana na wenzao. Hapo nikaelewa sababu za wazazi wangu kuniambia nipunguze matumizi ya simu.

Mimi nimepangiliwa muda maalumu wa kutumia simu ninapokuwa nyumbani. Muda huu ni saa kumi na moja jioni hadi saa kumi na mbili na nusu. Ninamshukuru mama yangu kwa kuupata muda huo ingawa ni mfupi. Baba yangu hapendi kabisa intaneti. Yeye husema ‘ningependelea kama intaneti isingekuwapo kabisa kwani unapotumia intaneti kwa muda mrefu unapoteza ujuzi wako wa kuzungumza kwenye jamii. Pia unajifunza upuuzi na huwi makini darasani kabisa’.

Kwa kiasi kikubwa, Bwana Musa alikubaliana na baba yangu kwamba intaneti ni kipingamizi darasani. Lakini alitutahadharisha kwa kusema ‘kuna umuhimu wa kutumia intaneti na mitandao ya kijamii kwani watu hupata ufahamu mkubwa wa mada tofauti na hujenga mahusiano mazuri ya kimataifa’.

Alitupa takwimu chache ambazo zilinishangaza. Kwanza alisema kwamba miaka miwili iliyopita, vijana walitumia takribani saa moja kila siku kwenye mitandao ya kijamii. Pia walikuwa na akaunti moja au mbili tu. Kwa hivyo walitumia muda huo kuangalia mitandao tofauti. Hivi sasa asilimia kubwa ya watu wanaotumia mitandao ya kijamii ni vijana. Alituuliza, ‘wangapi kati yenu mna uwezo wa kutotazama simu kwa zaidi ya saa zima?’ Hakuna hata mmoja wetu aliyenyoosha kidole. Halafu alituuliza, ‘wangapi kati yenu mna akaunti tano au zaidi kwenye majukwaa tofauti?’ Hapo karibu sote tulinyoosha vidole. Basi Bwana Musa alicheka na kusema, ‘mnaona, nyinyi vijana mnapenda kuwa sehemu tofauti wakati mmoja!’

Mimi ninapotumia intaneti hupenda kusoma hadithi tofauti kwenye tovuti za mitandaoni. Hizi huandikwa na waandishi ambao bado hawajajulikana na huwa nzuri sana. Pia huangalia filamu au vichekesho.

Ingawa ninapenda kupiga picha, kwa kawaida hupendelea kubandika picha za vyakula na si picha zinazoonyesha mahala nilipo na familia yangu kwani sitaki kujihatarisha. Bwana Musa alituonya na kusema kwamba, kuna hatia nyingi za kihaini zinazofanyika kwenye mitandao. Alitufahamisha kwamba, kwenye mitandao ya kijamii, vijana hukubali maombi ya urafiki kutoka kwa watu wasiowajua. Mimi sijawahi kufanya hivyo. Alisema kwamba mara nyingi vijana hutazama picha za watu wanaowaomba urafiki na kama zinavutia basi wao hukubali ombi la urafiki. Pia wakati mwingine hutazama kama wana marafiki wa pamoja na hao watu na kukubali urafiki. Kwa hakika uamuzi huu si mzuri kwani, kiukweli, wao hawawajui watu hawa na wanaweza kuwa waovu. Mambo haya huweza kuleta madhara mengi. Mfano ni hatari ya kuibwa na pia kupoteza usalama kutokana na vitisho tofauti. Bwana Musa alimalizia kwa kututahadharisha wote kwa kusema kwamba ni muhimu kuwa na nidhamu na pia kuwa makini.

Now answer the following questions in your own words, as far as possible. You should avoid copying word-for-word from the text.

- (a) Nini ajira ya Bwana Musa? [1]
- (b) Taja mambo **matatu** ambayo wanafunzi wengi hufanya katika simu zao za mkononi wakati wa asubuhi. [3]
- (c) Kwa sababu gani mhusika wa habari hii hupiga picha za vyakula? Taja sababu **mbili**. [2]
- (d) Mama ana hisia gani kuhusu kupiga picha chakula? [1]
- (e) Vijana wa zamani waliwasiliana kwa namna gani? Taja namna **mbili**. [2]
- (f) Tofautisha na fananisha maoni ya baba yake mhusika na Bwana Musa kuhusu intaneti. Taja maelezo **matano**. [5]
- (g) Kuna ushahidi gani kwamba vijana wanapenda kuwa sehemu tofauti wakati mmoja. Taja **mbili**. [2]
- (h) Mhusika anachukua hatua gani mtandaoni ili kujilinda? Taja hatua **mbili**. [2]
- (i) Umepata mawazo gani kuhusu Bwana Musa? Elezea maoni **mawili** kutoka kwenye habari uliyoisoma. [2]

[20 for Content + 5 for Language = 25]

- 4 Write a composition of about **120 words** in **Swahili** on **one** of the following topics:
- (a) ‘Advertising does more harm than good.’ Do you agree? Explain why.
- (b) ‘Our school holidays are too long and should be much shorter.’ Do you agree or disagree? Give reasons for your response.
- (c) Write a speech called ‘My vision for East Africa’.

[25]

**BLANK PAGE**

**BLANK PAGE**

---

Permission to reproduce items where third-party owned material protected by copyright is included has been sought and cleared where possible. Every reasonable effort has been made by the publisher (UCLES) to trace copyright holders, but if any items requiring clearance have unwittingly been included, the publisher will be pleased to make amends at the earliest possible opportunity.

To avoid the issue of disclosure of answer-related information to candidates, all copyright acknowledgements are reproduced online in the Cambridge Assessment International Education Copyright Acknowledgements Booklet. This is produced for each series of examinations and is freely available to download at [www.cambridgeinternational.org](http://www.cambridgeinternational.org) after the live examination series.

Cambridge Assessment International Education is part of the Cambridge Assessment Group. Cambridge Assessment is the brand name of the University of Cambridge Local Examinations Syndicate (UCLES), which itself is a department of the University of Cambridge.